


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

WAOMBAJI WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA KATIKA AWAMU YA NNE YA UDAHILI KWA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kuwa udahili kwa Awamu ya Nne katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2019/2020 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya Nne yameshatangazwa na vyuo husika.

Waombaji waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya nne na wale wa awamu zilizopita ambao bado hawajathibitisha udahili, wanasisitizwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimoja kuanzia tarehe 11 hadi 14 Oktoba, 2019. Jinsi ya kuthibitisha udahili ni kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuthibitisha.

Tume inasisitiza kuwa, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambazo waombaji walitumia wakati wa kuomba udahili katika vyuo walivyodahiliwa. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja katika awamu ya nne na awamu zilizopita ambao hawajathibitisha udahili imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

Aidha, waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kuthibitisha yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.

Imetolewa na:



Dkt. Telemu J. Kassile
Kny: Katibu Mtendaji
Tume ya Vyuho Vikuu Tanzania
11 Oktoba, 2019